OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA/UJIJI
SHULE YA SEKONDARI MASANGA
ANUANI YA POSTA: S.L.P 623 KIGOMA, **BARUA PEPE**: masangasecondaryschool@gmail.com
Mobile No. 0768338433 / 0713795600

MZAZI/MLEZI WA _____

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2020**

1.0. UTANGULIZI

Ninayofuraha kukutaarifu kuwa mwanao_____amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2021 katika shule hii ya Sekondari Masanga. Shule ipo umbali wa KM 3 magharibi mwa Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Kata ya Mwanga Kaskazini, Mtaa wa Mlole karibu na nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa (NHC).

Mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni tarehe 11.01.2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 25.01.2021. Kama hataripoti ndani ya muda huo, hatua kali za kisheria zitachukuliwa. Hivyo ni wajibu wa Mzazi kuhakikisha mwanafunzi anaripoti Shule kwa wakati.

2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1. SARE ZA SHULE

2.1.0. **WAVULANA**

- Suruali 2 za kaki zenye upana unaostahili, rinda 2 na zenye turn off chini(suruali za kubana (Modal) hazitaruhusiwa, Tai 2 na Shati 2 nyeupe zenye mikono mifupi.
- Viatu vyeusi vya ngozi, vyenye kamba na sori fupi
- Soksi nyeusi
- Mkanda mweusi wa ngozi
- T-shirt ya Blue Bahari yenye mikono mifupi na isiyo na maandishi
- Sweta rangi ya Kaki.

2.1.1**. WASICHANA**

- Sketi 2 za kaki ndefu zenye kuvuka magoti na zenye marinda ya boksi
- Shati 2 nyeupe zenye mikono mifupi na Tai 2
- Hijabu zinazoruhusiwa na kwa mujibu wa maelekezo ya dini ya kiislamu. Shati lazima liwe la mikono mirefu kwa wataovaa hijabu. Vilemba, Mitandio na Hijabu fupi haziruhusiwi
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye Kamba
- Soksi nyeupe
- T-shirt ya Blue Bahari yenye mikono mifupi isiyo na maandishi yoyote.
- Sweta la Kaki

2.2. SARE ZA MICHEZO

- ✓ Tracksuit ya Blue na Raba nyeusi kwa wote wavulana na wasichana

2.3. VIFAA VYA MASOMO (STATIONARIES)

- Madaftari 12 (Counter Book quire 2 au 3)
- Kamusi (Dictionary) kubwa 1 (ni lazima)
- Vitabu vya sanaa, Kalamu za kutosha, Rula na Mkebe wa Hisabati
- Begi la kubebea madaftari na vitabu (ni lazima kwa kila mwanafunzi)
-

2.4. MAMBO MENGINE MUHIMU WAKATI WA MASOMO

- Chakula cha wanafunzi wa kutwa.
- Nauli ya kwenda na kurudi kwa wanaokaa mbali
- Huduma za matibabu na usafiri pale mwanafunzi anapata changamoto ya magonjwa akiwa katika mazingira ya shule, ni jukumu la mzazi. Shule itatoa huduma ya kwanza tu pale mwanafunzi atakapozidiwa.
- Mahitaji mengine muhimu ya kibinadamu pamoja na vifaa vya usafi.

3.0. SHERIA NA TARATIBU MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu chini ya Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

3.1. MAMBO YA KUZINGATIA KUFUATIA SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE.

A. Heshima kwa Viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni **Lazima.**
B. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na Ratiba ya Shule ni **Lazima**
C. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation)
D. Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wa wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
E. Kutunza usafi wa mwili, Mavazi na Mazingira ya Shule ni jukumu la Mwanafunzi na hivyo ni **Lazima**
F. Kuzingatia Ratiba ya Shule wakati wote ni swala la Lazima kwa mwanafunzi
G. Kutunza Mali za Shule, za wanafunzi, na binafsi ni jukumu la mwanafunzi na hivyo ni **Lazima**

3.2. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi
ii. Uasherati na Ushoga
iii. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama Bangi, Cocaine, Kubeli, Ugoro, Pombe n.k
iv. Kupiga au Kupigana
v. Kuharibu kwa makusudi mali za Umma
vi. Kudharau Bendera ya Taifa
vii. Kupata Mimba (Ujauzito) AU Kumpa mwenzako Mimba (Ujauzito)
viii. Kutoa Mimba (Abortion)
ix. Kuoa au Kuolewa
x. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
xi. Kukataa amri Halali ya Mwalimu au adhabu kwa makusudi
xii. Kumiliki simu ya mkononi.

4.0. MAMBO MENGINE YA KUZINGATIA KWA MWANAFUNZI KUKAMILISHA USAJILI KAMILI

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporiti shuleni.
b) Fomu ya Maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi, Mkataba wa kutoshiriki Migomo, Fujo na Makosa ya Jinai.
c) Fomu ya Mzazi kukiri kukubaliana na Sheria, taratibu na maelekezo mengine yatakayotolewa na Shule.

5.0. MWISHO

Tafadhari soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

Nakutakia Maandilizi mema na Karibu sana Shule ya Sekondari Masanga



Emmanuel Steven Komba
Mkuu wa Shule

IJAZWE NA MZAZI/MLEZI

Mimi (Bwa/Bibi/Bi)_____ Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi _____, nimesoma na kuelewa Barua ya Mkuu wa shule ya Sekondari Masanga inayohusu Masharti ya Kujiunga na Shule. Nimezungumza na Mwanangu nae ameahidi kuyatekeleza masharti na sheria za Shule. Nakubali/Sikubali Mtoto wangu apewe nafasi katika Shule hii ya Sekondari Masanga. Hata hivyo naomba mtoto wangu awakiwa shuleni alelewe kwa maadili ya dhehebu la _____

Sahihi ya Mzazi/Mlezi _____

HISTORIA YA MWANAFUNZI

Jina la Mwanafunzi _____ tarehe ya Kuzaliwa_____

Anuani ya Nyumbani_____Kabila_____Dhehebu_____

Jina la Baba _____ (Hai/Marehemu). Dhehebu _____

Jina la Mama _____ (Hai/Marehemu). Dhehebu_____

Kazi ya Baba _____ Kazi ya Mama_____

MAJINA YA KAKA, DADA NA NDUGU WENGINE

S/No	JINA KAMILI	UMRI	S/No		UMRI
1			4		
2			5		
3			6		

Majina ya ndugu wengine wa karibu ambao tunaweza kuwasiliana nao kwa dharura yoyote inayomuhusu mtoto

S/No	JINA KAMILI	UMRI		NAMBA YA SIMU
1				
2				
3				
4				
5				

Jina la Mzazi/ Mlezi unayemtegemea: _____

Anuani: _____

Sahihi na Jina la Mwanafunzi: _____

Sahihi na JIna la Mzazi/Mlezi: _____

OR- TAMISEMI

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGOMA/UJIJI

SHULE YA SEKONDARI MASANGA

S.L.P 623, KIGOMA

ANUANI YA POSTA: S.L.P 623 KIGOMA, **BARUA PEPE**: masangasecondaryschool@gmail.com
Mobile No. 0768338433/0769361881/0713795600/0746600398

PHYSICAL EXAMINATION RECORDS FORM

(To be completed by Medical Officer in respect of all Form One/Five entrants)

Full name_____

Age _____

Sex ----------

Blood Count (Red or White) _____

Stool Examination _____

Urine Analysis _____

Syphilis Test_____

T. B. Test_____

Ears_____

Eyes_____

Chest_____

Spleen_____

Abdomen_____

ADDITIONAL INFORMATION Eg. Physical defects or impairments, infection chronic of family diseases.

_____

_____

_____

_____

I certify that, above the above person is **FIT/NOT FIT** to pursue as stated above

Medical Officer Name_____ Designation_____

Station_____ Signature_____

Stamp_____

NOTE: Medical Officer, at the time of examination, please examine the individual for any illness you note. This form should be returned to school with your acceptance. No any student will be enrolled without the certificate of physical fitness.